UTARATIBU WA KUNUNUA ZAO LA UFUTA KUPITIA SOKO LA BIDHAA TANZANIA (TMX)

1.0 Utangulizi

Katika msimu wa mauzo 2024/25 Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) kwa kushirikiana na halmashauri za mikoa, wilaya na wakurugenzi wa Halmashauri husika zitasimamia uendeshaji wa minada ya zao la ufuta katika ghala zinazotumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Katika msimu huu wa ufuta tani 100,000 zinakadiriwa kuuzwa kutoka mikoa ya Lindi, Mtwara, Manyara, Pwani, Dodoma, Katavi, Morogoro,Songwe na Ruvuma. Mauzo hayo yanalenga kuleta bei zenye ushindani wa haki, uwazi na kupunguza gharama za ununuzi wa zao la ufuta. Wanunuzi wote wa ndani na wa nje,wadogo na wakubwa wanakaribishwa kushiriki kwenye minada itakayoanza karibuni.

2.0 Majukumu ya Wanunuzi

i. Mnunuzi atatakiwa kuzingatia Sheria ya Stakabadhi za ghala sura 339 (RE) 2016 , Sheria ya Masoko ya Bidhaa 2015 na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya vyama vya ushirika katika msimu husika.

ii. Kujaza fomu ya kuridhia kununua ufuta kwa utaratibu uliowekwa na TMX na kuiwasilisha TMX kupitia mfumo wa kielektroniki wa mauzo ikiwa na nakala ya leseni ya biashara.

iii. Kupitia ‘Sales Catalogue’ na kuweka kiwango cha bei anayotaka kununua ufuta kwa njia ya kielektroniki wakati wa mnada. Kwa maelezo zaidi kuhusu namna ya kutumia mfumo wa kielektroniki wasiliana na TMX kupitia simu namba +255 713 298 314 au +255 685 319 433

iv. Kuweka fedha za Kitanzania ikiwa ni ‘’Deposit Margin’’ kama ifuatavyo:

Kiwango cha Dhamana (Tzs)	Idadi kwa Tani (MT)
20,000,000	Chini ya 20
50,000,000	20-50
70,000,000	51-80
100,000,000	81 na Zaidi
150,000,000	Nje ya Tanzania

kwenye akaunti ya malipo ya TMX:

Jina la Akaunti: **Tanzania Mercantile Exchange**
Benki: **CRDB**
Nambari ya Akaunti: **0150259178501**
Swift Code: **CORUTZTZ**

AU

Jina la Akaunti: **TMX Settlement**
AccountBenki: **NMB**
Nambari ya Akaunti: **20110041162**
Swift Code: **NMIBTZTZ**

- Maelezo zaidi kuhusu malipo haya wasiliana na TMX kupitia simu namba +255 22 2923700.

- Kiwango hiki kitarudishwa endapo mnunuzi aliyeshindwa kwenye mnada kutoa taarifa kuwa hataendelea kushiriki minada mingine na kuomba arejeshewe fedha hizo.

- Tozo zilizopo katika zao la ufuta (Tsh 198 kwa Kilo), ambapo zitalipwa na Mnunuzi ni kama ifuatavyo;

Aina ya Gharama	Tsh/Kilo
Chama cha Msingi	40
Chama Kikuu cha Ushirika	20
Vifungashio	16
CESS	30
Usafirishaji	40
Gharama za Mtunza Ghala	52
Jumla	**198**

- **NB:** *Endapo patakuwa na gharama nyingine zinazohusu Mkoa/Halmashauri husika zitakokotolewa na kuwekwa katika 'sales catalogue'*

v. Mnunuzi aliyeshinda kwenye mauzo atatakiwa kutekeleza yafuatayo

a. Kukamilisha malipo ya kiasi kilichoainishwa ndani ya masaa 48 siku za kazi toka mauzo kufanyika, yeye kutangazwa mshindi na kupokea *Invoice* kwa ajili ya malipo.

b. Malipo ya ushirika (**Union**, **AMCOS** na **wakulima**) kulipwa kwenye akaunti ya Union kama itakavyo ainishwa kwenye hati ya madai 'invoice'

c. Malipo ya gharama zingine ikiwa ni za Serikali kulipwa kwenye akaunti ya malipo ya TMX.

d. Endapo malipo hayatakamilika ndani ya masaa 48 , mnunuzi atatakiwa kulipa pamoja na 'adhabu' ya kiasi cha asilimia 5% ya fedha iliyobakia, kwa kipindi kisichozidi saa 24 za ziada (masaa 48 toka kutangazwa mshindi).

e. Endapo atashindwa kukamilisha malipo ndani ya masaa 48 basi mnunuzi huyo atahesabiwa kushindwa kulipia na kiasi kilichokuwa kimewekwa na mnunuzi huyo kama "advance" kitatumika kulipa fidia kwa wakulima waliokuwa wameuza ufuta husika na mnunuzi kushindwa kulipa.

vi. Mnunuzi aliyeshindwa kwenye mauzo

Kiwango hicho kitarudishwa kwenye akaunti ya mnunuzi ndani ya kipindi cha masaa 24 siku za kazi endapo mnunuzi huyo hajashinda kununua mauzo yalipofanyika na kutoa taarifa TMX kwa maandishi juu ya kurejeshewa fedha zake.

vii. Mnunuzi atatakiwa kuzingatia masharti na vigezo vya mnada wa mauzo ya ufuta kama yalivyotolewa katika mwongozo.

3.0 Hatua za Uuzaji Ufuta

i. Wanunuzi kujaza fomu ya kuridhia kununua ufuta kwa utaratibu uliowekwa na Soko la Bidhaa kwa njia ya kielektroniki.

ii. Wanunuzi wanaweka kinga ya dhamana kwenye akaunti ya malipo ilioainishwa.

iii. Mnunuzi aliyekamilisha hatua ya usajili na kinga Dhamana anaingizwa kwenye Mfumo wa Mauzo wa Kielektroniki wa TMX.

iv. TMX kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika kuhakiki taarifa na kuandaa Sales Catalogue kisha kutumwa kwa wadau mbalimbali.

v. Taarifa za Sales Catalogue zinaingizwa kwenye Mfumo wa mauzo wa TMX na Lots kupangwa kwa kuzingatia AMCOS/Uwingi wa mazao kufatia upangaji kwenye ghala kuu.

vi. Mfumo wa mauzo wa kielekroniki unafunguliwa kwa ajili ya wanunuzi wenye kupenda kufanya PreBid (Kuweka bei zao kabla ya mnada kuanza) bei hii itaonekana kwa mnunuzi tu mpaka pale muda wa mnada kuanza mfumo utakapofunguka.

vii. Minada kufanyika kwa njia ya kieletroniki (kwa ushindani) kwa wanunuzi kushiriki popote walipo kwenye eneo lenye mtandao na endapo kuna wanunuzi walifanya Pre-Bid,bei ya juu iliyopatikana ndio bei itakayoanzia kwenye lot husika kwa wanunuzi kuanza kushindana.

viii. Wanunuzi kushindana kununua kwa Lot (Lot moja ikiwa ni kiasi chote cha ufuta uliowasilishwa na AMCOS husika au mgawanyo kufuatia uwingi wa ufuta kwenye ghala). Lot moja ikitumia muda wa dakika 1 na endapo mnunuzi ameweka bei basi itarudi sekunde 40 mpaka ziishe bila mnunuzi mwingine kuweka bei.

ix. Chama Kikuu cha Ushirika kuingia kwenye mfumo wa TMX na kujaza taarifa ya kuridhia au kukataa bei zilizopatikana.

x. Taarifa kwa wadau wengine itatolewa na TMX kwa kielektroniki kwa kipindi kisichozidi nusu saa toka mnunuzi kujulikana ikionyesha

   a. Bei ya ufuta iliyonunuliwa, au

   b. Bei ya juu iliyoonekana endapo ufuta haukuuzwa

xi. Kwa mnunuzi ambaye hajafanikiwa kushinda/kununua na ameamua arudishiwe kiasi chake atarudishiwa fedha muda usiozidi masaa 24 siku za kazi toka taarifa ya uhitaji wa fedha zake kupokelewa TMX.

xii. Wanunuzi kuwekewa fedha zao ndani ya saa 48 toka mauzo kufanyika katika akunti za malipo kama zilivyo ainishwa kwenye hati ya madai ‘invoice’

……

IMETOLEWA NA AFISA MTENDAJI MKUU

SOKO LA BIDHAA TANZANIA

TAREHE 06/05/2024

Kwa maelezo ya jumla wasiliana na TMX kupitia: info@tmx.co.tz au namba ya simu ifuatayo;

+255 22 2923700.

Tanzania Mercantile Exchange PLC, P.O. Box 31632, Dar es Salaam, TANZANIA, Email: info@tmx.co.tz, website: www.tmx.co.tz